HALIUZWI

Jarida la NEMC

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

ISBN 0856 - 6933 | TOLEO NA. 008 | JULAI - SEPTEMBA, 2022

NEMC YATEKETEZA TANI 44 ZA VIFUNGASHIO VYA PLASTIKI VISIVYOKIDHI VIWANGO

Ndani:

- MAKAMU WA RAIS AFUNGUA MKUTANO WA UMOJA WA MATAIFA JUU YA TATHMINI YA HALI YA MAZINGIRA YA BAHARI
- OPERESHENI YA KAMATA MIFUKO YA PLASTIKI ISIYO RASMI YAZINDULIWA - NA MKUU WA MKOA DAR ES SALAAM, MAKALA
- MAKALA: BANDARI ZISIZOKUWA RASMI NA CHANGAMOTO KWENYE MAZINGIRA

@nemctanzania
NemcTVTanzania
www.nemc.or.tz

#MazingiraYetuUhaiWetu

YALIYOMO

003 Makamu wa Rais Afungua Mkutano wa Umoja Wa Mataifa Juu ya Tathmini ya Hali Ya Mazingira Ya Bahari

004 Jiji la Dar es Salaam Pitieni Mfumo Wa Maji ya Mvua Kubaini Waliounganisha Kiholela - Mhe. Jafo

005 Umuhimu wa Kutunza Vyanzo vya Maji kwa Uchumi Endelevu

006 Kamati ya Kudumu ya Bunge Yafanya Ziara Katika Dampo la Pugu Kinyamwezi na Kiwanda cha TOOKU Garments Jijini Dar es Salaam

08 Operesheni ya Kamata Mifuko ya Plastiki Isiyo Rasmi Yazinduliwa - Rc. Makala

009 NEMC Yatoa Miezi Sita kwa Muwekezaji Kuboresha Miundombinu ya Mazingira

009 Nemc kwa Kushirikiana na CTI Yaandaa Mafunzo ya Siku Moja

010 Umuhimu wa Kutunza Bahari kwa Manufaa ya Wote: Ni Kuhusiana na Umuhimu wa Ufanyaji wa Tathmini ya Athari Kwa Mazingira

011 Operesheni ya Kamata Mifuko ya Plastiki Isiyo Rasmi Yazinduliwa - Rc. Makala

012 NEMC Yashiriki Maonesho Katika Mkutano wa 20 wa Amecea

013 NEMC Yateketeza Tani 44 za Vifungashio vya Plastiki Visivyokidhi Viwango.

015 Waziri Jafo Afanya Ziara Katika Kiwanda cha Saruji cha Twiga

016 Vimiminika Taka Kichocheo cha Uchafuzi wa Mazingira na Mlipuko wa Magonjwa kwa Binadamu

017 Faida na Hasara za Makaa ya Mawe Katika Mazingira

018 Bandari Zisizokuwa Rasmi na Changamoto Kwenye Mazingira

019 Viwanda Endelevu, Uchumi Imara kwa Mazingira Safi na Salama

020 Kauli ya Mazingira

022 Kauli ya Mazingira: Katuni

UTANGULIZI

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilianzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira Na. 19 ya mwaka 1983 kama chombo cha kuishauri serikali juu ya masuala ya utunzaji endelevu wa Mazingira. Baraza lilianza kazi rasmi mwaka 1986. Sheria Na. 19 ya mwaka 1983 ilifutwa mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 (Sura 191) ambayo ilianzisha Baraza kwa mara nyingine.

Tangu kuanzishwa kwake, Baraza limekuwa likisimamia na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu suala zima la hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu nchini. Kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria hiyo, madhumuni na sababu za kuanzisha Baraza hili ni kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mazingira katika nyanja kuu nne ikiwa ni pamoja na:-

1. Kutekeleza shughuli za uzingatiaji na utekelezaji (enforcement and compliance) wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;
2. Kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) (Kuratibu, kufanya mapitio ya ripoti za TAM kutoka kwa wenye miradi na kufuatilia utekelezaji wake);
3. Kufanya tafiti za mazingira; na
4. Kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya uamuzi unaohusu mazingira na kusimamia kwa ujumla na kuratibu masuala yote yanayohusu Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sheria nyingine zozote zilizoandikwa.

BODI YA UHARIRI:

Mwenyekiti:
Dkt. Menan Jangu

Mhariri Mkuu:
Irene John

Wachangiaji:
Monica Sapanjo
Dalia Charles
Rose Mtui
Martha Kawishe
Pendo Kundya
Neema Mdimi
Hilda F. Mwakasungura

Msanifu Michoro:
Blasius Haule

MAKAMU WA RAIS AFUNGUA MKUTANO WA UMOJA WA MATAIFA JUU YA TATHMINI YA HALI YA MAZINGIRA YA BAHARI

Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Mpango wapili kutoka kushoto (walio kaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa mkutano wa tathmini ya hali ya Mazingira uliofanyika katika ukumbi wa JNICC jijini Dar es Salaam.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdori Mpango amefungua mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu tathmini ya hali ya mazingira ya Bahari ikiwemo masuala ya kiuchumi na kijamii. Mkutano umejumuisha washiriki kutoka katika mataifa mbalimbali duniani, ambapo Tanzania kwa mara ya pili imekuwa mwenyeji wa mkutano huo uliofanyika katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere Dar es salaam.

Mhe. Mpango amezipongeza jitihada zinazofanywa na taasisi kwa kupiga hatua katika utunzaji wa bahari kwa kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki, kudhibiti uvuvi wa kutumia mabomu kwa takribani asilimia 99 na kuongeza ulinzi na uangalizi katika shughuli za uvuvi. Pamoja na hayo ametoa wito wa kulinda bahari ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kudhibiti taka za plastiki na uchafuzi kwa ujumla wa bahari.

Pia amesisitiza kuwa inahitajika nguvu ya pamoja kutoka katika mataifa mbalimbali ili kuongeza juhudi katika utunzaji wa Bahari.

"Ni muda sasa muafaka wa kutafuta njia sahihi za kusimamia na kudhibiti shughuli zinazofanywa katika Bahari na jinsi ya kuleta usawa wa uhai wa bahari na ikolojia kwa maendeleo endelevu" alisema Mhe. Makamu wa Rais.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo alisema" Mkutano huo utasaidia kukuza uwezo kwa watafiti wa masuala ya mazingira jinsi ya kuratibu shughuli za uchumi wa bahari na pia Tanzania kuhakikisha kuwa jamii zetu zinatumia fursa ya Bahari katika kujenga uchumi na kuondoa umaskini.

Aidha Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa bluu na Uvuvi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Dkt. Aboud D. Jumbe amesema programu za Umoja wa Mataifa za uvuvi na uhifadhi wa bahari pamoja na taarifa sahihi za utunzaji wa bahari pamoja na kuchangia katika ukuaji wa fursa za kiuchumi ili kufikia maendeleo endelevu ya Bahari.

Kwa upande wake mwakilishi wa Umoja wa Mataifa kitengo cha mambo ya Bahari na Sheria ya Kimataifa Bi. Alice Hicuburundi amesema uelewa ni jambo muhimu zaidi katika kulinda na kutunza mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Bahari.

Kongamano hilo ni muhimu katika kuzijengea uwezo Nchi washiriki katika kusimamia na kuhifadhi Bahari kwa maendeleo endelevu.

JIJI LA DAR ES SALAAM PITIENI MFUMO WA MAJI YA MVUA KUBAINI WALIOUNGANISHA KIHOLELA - MHE. JAFO

Waziri wa Nchi Muungano na Mazingira Mhe. Dkt Selemani Jafo akizungumza watumishi wa DAWASA mara baada ya kutembelea hapo na kufanya ukaguzi wa mazingira.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo amelitaka Jiji la Dar es salaam kupitia kitengo cha mazingira kubaini waliounganisha mfumo wa maji taka kwenye mfumo wa maji ya mvua ili hatua kali za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

Ametoa kauli hiyo alipokuwa akifanya ziara katika Mkoa wa Dar es Salaam kujiridhisha na suala la uhifadhi, usimamizi na utunzaji wa Mazingira kwenye Soko la samaki la feri pamoja na ufukwe wa Oyster bay hususani kwenye mfumo wa maji ya mvua unaosimamiwa na DAWASA.

Amesema maeneo haya ni maeneo muhimu sana yenye mkusanyiko mkubwa wa wananchi hivyo maafisa mazingira kwa kushirikiana na NEMC wanapaswa kuongeza nguvu katika kuhakikisha misingi ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira inazingatiwa kwa kiwango kilichokusudiwa.

Aliongeza kwa kusema kuwa ni dhahiri kabisa baadhi ya wananchi wameunganisha mfumo wa maji taka kwenye mfumo wa maji ya mvua unaopeleka maji baharini hali inayohatarisha maisha ya wanadamu na viumbe hai hivyo ni vema watu hao kuacha tabia hio na wale wanaokiuka kuchukuliwa hatua za kisheria.

> " Ni dhahiri kabisa baadhi ya watu wameunganisha mfumo wa maji taka kwenye mfumo wa maji ya mvua, tuko hapa katika bahari, ukiangaalia unasikia harufu mbaya, unaona mpaka kinyesi, hii haikubaliki." *Mhe Dkt. Selemani Jafo.*

Aidha aliwataka maafisa mazingira wa Jiji la Dar es salaam kuhakikisha jukumu hilo linatekelezwa kwa haraka na wakati ili kunusuru mlipuko wa magonjwa yanayoweza kutokea na hali za wafanyabiashara pamoja na wananchi wanaokwenda kupumzika eneo la fukwe kuwa hatarini.

Katika hatua nyingine amewapongeza wafanyabiashara wa soko la feri kwa usafi wa mazingira na kujali uhai wa misitu kwa kutumia teknolojia ya gesi kukaangia samaki zao, na kuitaka Manispaa ya Kinondoni, kwa kushirikiana na DAWASA na NEMC ndani ya mwezi mmoja kukamilisha mchakato wa tathmini ya athari kwa mazingira eneo la ufukwe ili waweze kujenga vyoo.

makala

UMUHIMU WA KUTUNZA VYANZO VYA MAJI KWA UCHUMI ENDELEVU

Vyanzo vya maji ni yale maeneo ambayo maji huanzia hapo kama vile chemichemi, mito, maziwa, kisima, mabwawa na bahari. Na kupitia vyanzo vya maji hivi tunapata chakula, biashara, utalii pamoja na nishati.

Tanzania imejaliwa kuwa na vyanzo vya maji vya aina mbalimbali. Vyanzo hivyo ni pamoja na mito, maziwa, ardhi oevu na maji chini ya ardhi. Lakini hivi karibuni kumekuwapo na uharibifu mkubwa wa vyanzo hivi vya maji kutokana na ukataji wa miti katika vyanzo vya maji kwa ajili ya kuni pamoja na kuendesha kilimo na ufugaji katika maeneo hayo.

Zipo njia mbalimbali za kutunza vyanzo vya maji Kwa ajili ya uchumi endelevu ni kama vile; kuepuka kutupa takataka katika vyanzo vya maji. Takataka zinapotupwa katika vyanzo vya maji huziba chemichemi hizo na kusababisha zikauke na hapo ndipo maji hukoma kutoka na vyanzo hivi hupotea au kutoweka kabisa, hali inayosababisha vyanzo kukauka na kuweza kuleta hata ukame. Ukame huharibu sana ukuaji wa uchumi wa Taifa lolote lile kwa kupoteza nishati mbalimbali ambazo zingepatikana kupitia maji hayo.

Sio hivyo tu vyanzo vya maji vinapokauka vinasababisha mifugo kukosa maji na hivyo inakufa na kusababisha hasara na kuathiri uchumi wa mwenye mifugo, jamii na Taifa kwa ujumla, hivyo inarudisha nyuma juhudi za kufikia uchumi imara na endelevu.

Njia nyingine ni kuepuka uvuvi haramu na kutumia njia salama za uvuvi wa samaki. Uvuvi haramu ndiyo chanzo kikubwa cha kuharibu mazingira na mifumo ikolojia ya ziwa au chanzo kingine cha maji. Hii ni pamoja na kupungua kwa idadi ya makundi ya samaki na hata kupotea kabisa kwa aina nyingine za samaki ambazo zilisababishwa na baadhi ya athari kubwa sana ambazo zimesababishwa na uvuvi haramu wa muda mrefu. Uvuvi haramu na usiofuata kanuni za utunzaji wa mazingira unakadiriwa kuwa ni tani milioni 26 kwa mwaka au sawa na moja ya tano ya samaki wote wanaovuliwa kote duniani na mbali ya kupora raslimali za jamii pia unachangia katika uharibifu wa mazingira ya bahari na kuathiri viumbe. Utumiaji wa kemikali katika uvuvi wa samaki hupelekea uharibifu mkubwa wa chemichemi katika vyanzo vyake maana kemikali hizo hufanya vyanzo hivyo vya maji kuziba.

Aidha, njia yingine ni kuepuka utupaji taka za viwandani zinavyoingia katika vyanzo vya maji. Katika mchakato wa kikemikali unaotokea wakati wa kuharibika au kuchakaa kwa plastiki unaotokana na kupigwa jua, upepo na mawimbi, plastiki hizo huvunjika vunjika katika vipande vidogo vidogo (microplastic) vinavyowezwa kuliwa na viumbe vya bahari na kuwaletea madhara ambayo pia hufikia mwanadamu kwa kuwala viumbe hao.

Athari za uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji na mazingira umekuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa jamii nyingi sana duniani na hata katika nchi yetu. Utupaji taka usiozingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira umesababisha vyanzo vya maji kuziba hivyo kukwamisha shughuli za uzalishaji na kupoteza kipato kuanzia ngazi ya familia, jamii, Taifa na dunia kwa ujumla.

Vyanzo vya maji vinapoharibiwa kwa ajili ya shughuli za kibinadamu zisizozingatia utunzaji wa mazingira uharibifu mfumo mzima wa utiririshaji maji na kuleta uhaba mkubwa wa maji na hata kupelekea shughuli za kibiashara zinazotegemea maji kusimama. Shughuli kama kilimo cha umwagiliaji, uvuvi na usafirishaji wa majini haziwezi kuendelea kama vyanzo vya maji vitaharibiwa. Hii kwa sababu uendeshwaji wa shughuli hizi unategemea maji.

Uchafuzi wa bahari wa plastiki unahatarisha afya ya bahari yenyewe, viumbe vyake, usalama wa chakula, afya za binadamu, utalii wa pwani na inachochea mabadiliko ya tabianchi ambayo hupelekea kukauka kwa vyanzo vya maji kwa kuwa taka za kemikali zitokazo viwandani zinaweza kuziba chemichem za maji.

Sio hivyo tu bali hata nishati za umeme zinazozalishwa majini haziwezi kuwa za uhakika ikiwa vyanzo vya maji vitaharibiwa na kusababisha maji kupungua. Maji yanapopungua yanafanya uzalishaji wa nishati upungue.

Serikali imesisitiza umuhimu wa utunzaji wa vyanzo vya maji kwa faida ya wananchi wote nchini na kwa ajili ya uchumi endelevu . Tukitunza vyanzo vya maji mazingira yetu yatakuwa salama na viumbe pia tutapunguza kupotea kwa viumbe wa majini na kuongezeka kwa idadi ya viumbe hao. Uchafuzi wa vyanzo vya maji unaweza ukasababisha madhara mbalimbali kwa viumbe wa majini, binadamu na mazingira kwa ujumla.

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YAFANYA ZIARA KATIKA DAMPO LA PUGU KINYAMWEZI NA KIWANDA CHA TOOKU GARMENTS JIJINI DAR ES SALAAM

Kamati ya kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira wakiwa katika kiwanda cha Tooku Garments Tanzania wakati wa ziara yao Mkoani Dar es Salaam.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira imefanya ziara katika Dampo lililopo Pugu Kinyamwezi na Kiwanda cha TOOKU Garments jijini Dar es Salaam kukagua utekelezaji wa Sheria ya Mazingira na kupata muda wa kujifunza shughuli mbalimbali za uzalishaji na uhifadhi wa Mazingira katika maeneo hayo.

Aidha, mara baada ya kutembelea katika Kiwanda cha TOOKU Garments imeutaka uongozi wa Mamlaka ya Ukanda Maalumu wa Uwekezaji (EPZA) kuboresha miundombinu ya kimazingira katika eneo hilo ili kuweza kuwavutia na kuwashawishi wawekezaji wengi zaidi.

Akizungumza wakati wa ziara ya Kamati hiyo iliyotembelea Dampo la Pugu Kinyamwezi na baadae Mamlaka ya Ukanda Maalumu ya Uwekezaji (EPZA), Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. David Kihenzile alisema hatua hizo zote za uhifadhi na utunzaji wa mazingira ni muhimu sababu zinazolenga kuhakikisha afya ya jamii nzima ni salama.

Akiwa na Kamati hiyo katika dampo la Pugu Kinyamwezi, Kihenzile alisomewa ripoti ya utendaji kazi wa Dampo na Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala Mhe. Amani Mafuru aliyebainisha kuzidiwa kwa dampo hilo kutokana na wingi wa taka zinazozalishwa katika Jiji la Dar es Salaam ililinganishwa na uwezo wa dampo.

"Tumejionea changamoto lukuki ambazo zinalikabili dampo hili, kimsingi sisi kama kamati tumeona kuna kila sababu ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa upande wa Mazingira kuweka mkono wake mahali hapa na kulisaidia Jiji la Dar es Salaam ambalo linaoekana wazi kuwa limezidiwa nguvu" alisema Mhe. Kihenzile.

Mhe. Kihenzile pamoja na mambo mengine aliongezea kuwa Serikali ikiweka mkono wake kwa kiasi kikubwa itasaidia kuokoa maisha ya wananchi waliopo jirani na dampo hilo kutokana na athari zitokanazo na dampo ikiwemo hewa chafu.

Aidha kamati hiyo pia ilishauri kuona namna gani afya za wananchi waliopo karibu na dampo pamoja na kiwanda zinalindwa lakini pia wafanyakazi wanaotoa huduma katika dampo hilo wanapewa mafunzo na vifaa vya kujikinga.

Kamati ya kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira wakiwa katika ziara ya kutembelea dampo la Pugu Kinyamwezi katika mkoa wa Dar es Salaam.

Kauli ya Mazingira Yetu



OPERESHENI YA KAMATA MIFUKO YA PLASTIKI ISIYO RASMI YAZINDULIWA - RC MAKALA

Mkuu wa mkoa wa Dar es salaam Mhe. Amos Gabriel Mkalla akiwa katika kikao na watumishi wa NEMC ofisini kwake jijijni Dar es salaam ambapo alitoa tamko la katazo la vifungashio vya plastiki.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amos Makala amezindua rasmi Operesheni ya Kamata Mifuko ya Plastiki itakayoanza siku ya Jumatatu ya Agosti 29, 2022 kwenye Masoko yote ya Jiji la Dar es salaam.

Operesheni hiyo imezinduliwa katika kikao kazi kilichofanyika katika ukumbi wa LAPF Millenium Tower kilichohusisha viongozi wa masoko yote ya Mkoa wa Dar es Salaam, kwa lengo la kutekeleza Agizo la Makamu wa Rais wa wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Philip Mpango la kutaka kila Mkoa kuendesha operesheni ya kutokomeza mifuko ya plastiki ili kufikia azma ya pamoja ya kuhifadhi na kulinda mazingira.

NEMC YATOA MIEZI SITA KWA MUWEKEZAJI KUBORESHA MIUNDOMBINU YA MAZINGIRA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limetoa miezi sita kwa muwekezaji wa makaa ya mawe kutoka kampuni ya Ruvuma Coal Limited kuboresha miundombinu ya mazingira, ikiwa ni pamoja na kujenga ghala la kuhifadhia makaa ya mawe wakati yakisubiri kusafirishwa nje ya nchi ili kuepukana na changamoto zinazoweza kujitokeza na kuleta athari za mazingira, binadamu, wanyama na mimea.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt Samuel Gwamaka mnamo tarehe ... alipofanya ziara ya kikazi katika Bandari ya Mtwara kwa lengo la kukagua miundombinu ya kusafirisha makaa ya mawe na kukuta uharibifu wa mazingira uliosababishwa na muwekezaji huyo.

Mkurugenzi Mkuu alisema uwekezaji wa makaa ya mawe unatakiwa kuzingatia Sheria ya Mazingira na Kanuni zake ili kuepusha athari zinazoweza kutokea.

Alisema "uwekezaji huu ni mzuri sana, tena una tija kubwa sana kwa Taifa letu, lakini lazima uzingatie Sheria ya Mazingira. Mkaa unapokuwa chini ya Ardhi hauna athari, ila unapoutoa unakuwa tayari umeweka wazi yale madini tembo, chuma, zinki na madini mengine yanayoweza kutengeneza tindikali kama sulphur ambayo sio rafiki kwa maisha ya binadamu na mimea" Dkt Gwamaka

Aidha ameainisha madhara yanayoweza kutokea kwa hali hiyo ya vumbi la mkaa kuendelea kuwa ni madhara ya afya kutokana na vumbi, uchafuzi wa hewa asilia pamoja na kuharibiwa kwa ikolojia ya ardhi inayoweza kuharibu mimea na viumbe hai.

Naye Meneja wa Kanda ya Kusini inayojumuisha Mikoa ya Mtwara, Ruvuma na lindi Mhandisi Boniphace Guni alipozungumza amesema atahakikisha maelekezo yote hayo yanatekelezwa ikiwa ni pamoja na kusimamia suala zima la utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 inayosisitiza ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira kabla ya uwekezaji.

Mkurugenzi Gwamaka katika ziara yake hiyo ametembelea eneo la Bandari ya Mtwara, eneo la STAMICO na eneo lililoko nje ya Bandari ambayo muwekezaji wake ni kampuni iitwayo SEBDO.

NEMC KWA KUSHIRIKIANA NA CTI YAANDAA MAFUNZO YA SIKU MOJA

NI KUHUSIANA NA UMUHIMU WA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Shirikisho la wenye viwanda Tanzania (CTI) wameandaa mafunzo ya siku moja yahusuyo umuhimu na uelewa wa ufanyaji wa tathmini ya athari kwa Mazingira katika viwanda wanavyovisimamia au kufanya kazi.

Akifungua mafunzo hayo yaliyofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa NEMC, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Baraza Dkt. Menan Jangu amesema lengo la mafunzo hayo ni kubadilishana uelewa na uzoefu katika uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na kanuni zake, kubwa ikiwemo umuhimu wa ufanyaji wa Tathmini ya athari kwa mazingira ili kuweza kukabiliana na changamo zinazoweza kujitokeza.

"Sisi NEMC, wadau wetu wakubwa ni wenye viwanda, na wajibu mkubwa tulionao kwenu ni kuhakikisha kwanza wanauelewa juu ya uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, lakini pia wanatambua umuhimu wa ufanyaji wa tathmini ya athari kwa Mazingira ili kuweza kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza lakini pia tuweze kutunza na kuyahifadhi mazingira" Amesema Dkt. Menan.

Ameongeza kuwa faida kubwa za ufanyaji wa tathmini ya athari kwa mazingira ni kukupatia mwelekeo wa kimazingira wa jinsi gani kiwanda chako kitekeleze shughuli zake ili kuepuka changamoto zinazoweza kutokea kubwa zikiwemo za uchafuzi na uharibifu wa mazingira na pia kuhakikisha maendeleo endelevu.

Naye Mkurugenzi wa Sera kutoka Shirikisho la viwanda Tanzania (CTI) Ndg Akida Mnyenyelwa amesema, mafunzo haya yatawasaidia sana wenye viwanda kutekeleza wajibu wao wa kimazingira kwa weledi ili kuepukana na changamoto zinazoweza kutokea hasa ikizingatiwa suala la uchafuzi wa mazingira limekuwa kero kubwa katika Nchi ya Tanzania.

"Niwaombe Wana CTI wenzangu, tutumie fursa hii tuliyoipata leo kubadilishana uzoefu wa uhifadhi wa mazingira ili tuweze kupata elimu juu ya utunzaji wa Mazingira, Lakini pia ili tuweze kupata majibu ya maswali yetu yote ya Kimazingira tuliyonayo, hawa wenzetu wa NEMC ni wataalam wa Mazingira hivyo tutumie fursa hii muhimu ili kwa pamoja tuweze kutunza na kuhifadhi Mazingira" Ameongeza Ndg. Akida.

Mafunzo haya ni ya siku moja yenye lengo la kujenga uelewa juu ya umuhimu wa ufanyaji wa tathmini ya athari kwa mazingira.

makala

UMUHIMU WA KUTUNZA NA KUHIFADHI BAHARI KWA MANUFAA YA WOTE



Kila mwaka huadhimishwa Siku ya Bahari Duniani ifikapo tarehe 8 Juni, ambapo mwaka 2022 imeongozwa na kauli mbiu isemayo "Kuhuisha hatua ya pamoja kwa ajili ya bahari" ikitaka kuhamasisha serikali, mashirika, asasi za kiraia na wadau wote kuchukua hatua kwa pamoja ili kuilinda bahari na rasilimali zake kwa faida ya kizazi cha sasa na vijavyo. Siku hii ilitangazwa na Umoja wa Mataifa mnamo mwaka 1992.

Umoja wa Mataifa unakumbuka kwamba zaidi ya watu bilioni tatu idadi kubwa wakiwa katika nchi zinazoendelea, maisha na uchumi wao unategemea rasilimali kutoka Baharini na Pwani. Pia bahari zinasongwa na uchafuzi wa aina mbalimbali ikiwemo taka za plastiki, ambazo zinaonekana kila kona iwe kwenye matumbawe hadi kwenye kina kirefu cha bahari.

Ikiwa bahari itaendelea kujazwa kwa uchafu wa kila aina kutokana na shughuli za kibinadamu za aina mbalimbali italeta athari kubwa sana katika maendeleo ya afya za watu, uchumi wao pamoja afya ya bahari yenyewe ikiwa ni pamoja na viumbe vyake.

Taka nyingi za plastiki zinaonekana katika maeneo ya fukwe na kuharibu mandhari nzuri kwa ajili ya mapumziko kwa kuwa na upepo mwanana wa bahari. Fukwe pia huwawezesha wakazi wa maeneo ya Pwani kushiriki michezo mbalimbali ikiwemo kuogelea, matembezi, riadha, na burudani zingine zinazopatikana katika fukwe.

Aidha miamba ya Matumbawe ambayo ni baadhi ya mifumo ya ikolojia muhimu na ya thamani Zaidi katika Sayari hii ya Dunia. Miamba ya Matumbawe inafunika karibu asilimia 0.1 ya sakafu ya bahari hivyo bahari inapoharibiwa hufanya miamba ya matumbawe kupotea na kuharibu sakafu ya bahari na makazi ya viumbe hai wa majini.

Pamoja na kuwa bahari ina faida nyingi kwa ajili ya maendeleo yetu kiuchumi, kijamii na kisiasa lakini sisi binadamu ndio tunaiochafua na kuiharibu kutokana na shughuli mbalimbali na utupaji hovyo wa taka usiozingatia utunzaji na uhifadhi wa bahari zetu. Taka nyingi za majumbani na viwandani zinatupwa baharini kila siku na kuathiri sana hali ya bahari pamoja na viumbe vyake vyote.

Nchi ya Tanzania imebarikiwa kuwa na uwanda mkubwa wa Bahari unaotumika kwa michezo mbalimbali kama vile, kuogelea, mpira wa mikono wa ufukweni (Beach Volleyball), Mbio za pikipiki za majini n.k. na vyote vimekuwa vivutio vikubwa cha vya utalii katika Taifa letu. Katika maeneo ya fukwe za bahari pia kuna maeneo yaliyotengenezwa kwa ajili ya michezo ya watoto na migahawa ya vyakula ambavyo hutia hamasa watu kutembelea maeneo haya.

Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wageni mbalimbali na wakazi wa mikoa mingine ambapo ukanda wa bahari umepita pia wanapata fursa ya kufanya utalii wa bahari kwa kutembelea visiwa vilivyopo katika bahari ya Hindi vikiwemo Bongoyo, Pungavini, Mwakatumbe, Mbudya na Sinda.

Aidha vyakula safi vya asili ikiwemo samaki, vinywaji pamoja na michezo ya kwenye maji kwa kutumia vifaa maalum zikiwemo boti ni burudani tosha kwa wakazi wa maeneo ya ukanda wa bahari na wageni mbalimbali wanazozipata kwa uwepo wa fukwe.

Zaidi ya asilimia 80 ya uchafu ndani ya maji unatoka ardhini, ikiwa tunaendelea kuijaza bahari na taka, itaendelea kuturudishia kwa mawimbi na upepo takataka hizo, na hii itaendelea kuleta athari zaidi katika Mazingira yetu.

Duniani, tani milioni nane za plastiki huingia baharini kila mwaka, hasa kwa njia ya vifaa vya ufungaji, chupa na sigara. Uzalishaji wa plastiki duniani umeongezeka mara mbili zaidi ya miaka kumi na tano iliyopita, ikifikia zaidi ya tani milioni mia tatu kwa mwaka na kuanza kutishia hali ya usalama wa bahari na viumbe vyake pamoja na afya ya binadamu.

Aidha takataka nyingi katika fukwe za bahari hutoka kwa wenyeji (yaani wakazi wa maeneo hayo) Hivyo elimu zaidi juu ya ufahamu kuhusu matumizi ya plastiki na kutunza bahari ipewe kipaumbele katika jamii na kuijengea jamii uelewa wa kuwa na bahari salama kwa ajili ya manufaa ya wengi na kwa uchumi endelevu.

Ili kutunza ubora wa bahari ni vyema kufahamu hali yake ya sasa, na kuelewa athari za vitendo vya mwanadamu na mabadiliko ya tabianchi dhidi yake. Bahari zilizotunzwa vyema ni muhimu kwa kuendeleza maisha kwenye sayari hii ya Dunia, mathalani ikiwa ni kudhibiti tabianchi, kuzalisha chakula chenye lishe bora, na kuwa chanzo cha ajira zinazonufaisha mamilioni ya watu. Hivyo tusipotunza bahari faida na uzuri wote huo ambao tungeupata unakuwa kinyume chake.

"BAHARI SALAMA, JUKUMU LANGU"

Bahari iliyochafuliwa na mafuta kutoka katika meli kubwa

Bahari iliyochafuliwa na taka ngumu mbalimbali haswa za plastiki

ELIMU YA MAZINGIRA KIVUTIO MKUTANO WA AMECEA

Watumishi wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC wakiwa wamejipanga tayari kwa ajili ya kutoa elimu ya mazingira katika mkutano wa AMECEA uliofanyika jijini Dar es salaam.

Elimu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira inayotolewa na NEMC imeonekana kuwavutia wengi katika Mkutano wa 20 wa AMECEA uliofanyika katika ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu J.K Nyerere Jijini Dar es salaam.

Elimu hiyo iliyohusisha tathmini ya athari kwa mazingira, utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria za mazingira, masuala ya tafiti kwenye mazingira, pamoja na huduma za kisheria imetolewa kwa Mataifa tisa yaliyoshiriki kwa lengo la kujadiliana athari za maendeleo katika mabadiliko ya tabianchi.

Akiongea na vyombo vya habari, Askofu Flavian Kassala wa Jimbo la Geita amesema kazi inayofanywa na NEMC kuhusiana na mazingira ni muhimu sana kwani imerahisisha ufuatiliaji na uzingatiaji wa sheria katika utekelezaji wa jukumu lake kuu la utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

Akielimisha Umma huo kipengele cha tathmini ya athari kwa mzingira mtaalam kutoka NEMC Bi. Suzan Chawe amesema ni vizuri kuzingatia taarifa sahihi za hali ya hewa kutoka mamlaka husika katika uandaaji wa ripoti za TAM kwa miradi ya maendeleo ili kuepukana na changamoto za kimazingira zinazoweza kutokea kubwa ikiwa mabadiliko ya tabia Nchi.

Nchi zilizoshiriki katika Mkutano huo ni Eritrea, Ethiopia, Kenya, Malawi, Sudan, Afrika ya Kusini, Uganda, Zambia na Tanzania ambayo kwa mwaka 2022 ndio mwenyeji.

> "Elimu ya mazingira yapaswa kuzingatiwa sana kwani ndio msingi imara wa upangaji na utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa kuzingatia athari zinazoweza kutokea katika suala zima la mabadiliko ya tabia Nchi".
>
> *alisema Askofu Flavian Kassala*

makala

NEMC YASHIRIKI MAONESHO KATIKA MKUTANO WA 20 WA AMECEA

Baraza limeshiriki katika maonesho ya mkutano wa 20 wa Kimataifa wa shirikisho la Baraza la Maaskofu Katoliki Kanda ya Afrika Mashariki na Kati (AMECEA) uliofanyika katika ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere mnamo tarehe 11 hadi 13 Julai, 2022.

Mkutano huo wa Shirikisho la Mabaraza ya Maaskofu Katoliki *(Association of Member Episcopal Conference in Eastern Africa {AMECEA})* linalojumuisha nchi tisa za Kanda ya Afrika Mashariki na Kati. Lengo la kufanyika kwa mkutano huu lilikuwa kujadili athari za mazingira katika maendeleo shirikishi ya binadamu *(Environmental Impact on integral Human Development)* hususani namna sahihi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kutunza na kuhifadhi Mazingira.

Akihutubia katika mkutano huo uliojumuisha nchi za Tanzania, Ethiopia, Kenya, Malawi, Eritrea, Sudani, Sudani ya Kusini, Uganda na Zambia mgeni rasmi ambaye pia ni Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amelipongeza Baraza la Maaskofu kwa kuja na wazo pevu la kukutana kwa pamoja kama taasisi za dini na kujadiliana masuala ya mazingira hususani uhifadhi na utunzaji wake kwa mstakabali wa maendeleo ya nchi washiriki wa Mkutano wa AMACEA.

Mhe. Rais amesema "Niwapongeze Kanisa Katoliki kuamua kujadiliana na kutekeleza kwa vitendo mambo ambayo tumeamrishwa na Ulimwengu kupitia malengo endelevu 17 ya Dunia (Sustainable Development Goals). Hii ni pamoja na malengo ya Umoja wa Afrika ambayo mengi yanagusa masuala ya Mazingira kwa namna moja ama nyingine"

Amerejea Sera na Sheria ya Mazingira ambayo nchi ya Tanzania kupitia Bunge lake tukufu imepitisha ikiwa ni hatua ambazo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imechukua hadi sasa katika kuhakikisha suala la mazingira linapewa kipaumbele. Maeneo yaliyotiliwa mkazo katika sera hiyo ni pamoja na kulinda vyanzo vya maji na misitu, kusisitiza upandaji wa miti na kuhakikisha miji yote inakuwa na mpango wa kusafisha mazingira kila wiki hasa katika maeneo ya viwanda na biashara, na makazi ya watu. Ameeleza Mhe Rais Samia.

Vilevile, katika hotuba yake aliainisha waalikwa wake kuwa ni viongozi wa dini, asasi za kiraia, viongozi wa Serikali pamoja na wadau wa mazingira na kukiri kuwa ni hazina kubwa Mungu aliyoiachilia katika kujadili suala zima la mazingira. Aliahidi kama nchi kushirikiana kwa pamoja katika kutekeleza azma hiyo ya utunzaji wa mazingira ili kuweza kurithisha kwa kizazi kijacho.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muugano na Mazingira, Mhe.

Inaendelea Uk. 12 >>

NEMC YATEKETEZA TANI 44 ZA VIFUNGASHIO VYA PLASTIKI VISIVYOKIDHI VIWANGO

Mkurugenzi mkuu wa NEMC Mhandisi Dkt. Samuel Gwamaka Mafwenga

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) leo limeteketeza tani 44.4 za vifungashio vya Plastiki visivyokidhi viwango.

Akizungumza katika zoezi hilo la uteketezaji Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Samuel Gwamaka amesema vifungashio hivi ni vile visivyopaswa kuingia sokoni kwani havikidhi vigezo stahiki vilivyowekwa na Serikali kwa ajili ya matumizi hayo.

Ameongeza kuwa ni vema umma wa watanzania ukaelewa umuhimu wa zoezi hili na kushirikiana kwa pamoja kuhakikisha linatekelezeka kwa ufanisi na kiwango kilichokusudiwa.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Godwin Gondwe alipozungumza amekiri kushirikiana na NEMC katika kutekeleza agizo hilo la Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Philip Mpango la kuteketeza vifungashio visivyokidhi vigezo kwenye Halmashauri yake, na kuwataka Mameneja wa Masoko wote kuhakikisha wanasimamia Masoko vifungashio hivyo visitumike.

> "Leo tuko hapa, tunateketeza vifungashio Tani 44.4, hivi vifungashio havipaswi kuingia sokoni na ndio maana tunachukua jukumu la kuviteketeza Ili kuwaonesha wengine kwamba havipaswi kuwa kwenye Mazingira kwa sababu vikiingia huathiri ustawi wa jamii."
>
> Amesema Mkurugenzi Dkt. Gwamaka.

>> Inatoka Uk. 10

Selemani Jafo alipozungumza, kwa kutia mkazo suala zima la uhifadhi na utunzaji wa mazingira na kuagiza wakuu wa Mikoa wote kuhakikisha wanaimarisha usafi kwenye maeneo yao. Hii ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa maagizo ya Mhe Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania awamu hii ya sita ya kutaka usafi ufanyike kila wiki mara moja kwenye Mikoa yetu yote nchini. Alisema "Mikoa yote anapaswa kuhakikisha anatekeleza agizo la Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuandaa mpango mkakati wa kufanya usafi kila wiki kwenye maeneo yao".

Katika mkutano huo ambao azma yake kuu ilikuwa ni mazingira, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kama mdau mkubwa wa mazingira, lilishiriki kwa kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na suala zima la uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

Elimu iliyotolewa na wataalam kutoka idara mbalimbali za Baraza ilihusisha umuhimu wa uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 pamoja na kanuni zake, umuhimu wa kufanya tathmini ya athari kwa mazingira, umuhimu wa kuhifadhi, kutunza na kulinda mazingira. Hii ni pamoja na umuhimu katika masuala mazima ya tafiti kupitia miradi, programu mbalimbali ili kubaini changamoto, fursa na kuchukua hatua stahiki katika kuhifadhi, kulinda na kutunza mazingira.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazigira (NEMC) Dkt. Samuel Gwamaka katika kuzungumzia masuala ya mazingira katika maonesho hayo, alionesha kufurahishwa na Mkutano huo wenye lengo chanya kuhusiana na Uhifadhi na Utunzaji wa Mazingira nchini, hasa ikizingatiwa jukumu la Bazara katika kutekeleza na kusimamia Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 pamoja na kanuni zake. Mha. Dkt Gwamaka alisema "Sisi (NEMC) maeneo haya ni yetu katika kuhakikisha Sheria ya Mazingira inazingatiwa kwenye Mipango yote endelevu ya Nchi hii kuhusiana na Mazingira. Kunapokuwa na majadiliano yeyote yanayohusu Mazingira, sisi ndio wadau wakubwa katika sekta hiyo".

Aidha amewataka wananchi pia kuhakikisha wanaunga mkono wito uliotolewa na Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutambua amana kubwa ya ardhi na hewa safi tuliyojaliwa na Muumba wetu. Vilevile alisisitiza kulinda na kutunza mazingira kwa kufanya usafi ili kuepusha Taifa na majanga ya magonjwa ya mlipuko na magonjwa ya kuambukizwa lakini pia kuepukana na athari zinazoweza kutokea kwa kutolinda Mazingira ikiwemo athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Katika hatua nyingine Baraza pia liliwakaribisha wadau mbalimbali kutoka nchi tisa za wananchama wa shirikisho la Baraza la Maaskofu Katoliki waliokuwa wakitembelea kwenye banda la maonesho ya mkutano wa 20 wa (AMECEA) ili kutoa maoni na ushauri wa mwenendo mzima wa jinsi gani jukumu la kusimamia sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 linatekelezeka kwa nchi mwenyeji wa shirikisho hilo kwa mwaka 2022 ambayo ni Tanzania.

Maoni hayo yalihusisha Pongezi kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa na chombo kinachosimamia na kushughulikia masuala ya Utunzaji na Uhifadhi wa Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004. Pia pongezi kwa kupiga marufuku mifuko ya plastiki na kuwa na kiongozi anayetambua umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa mazingira hali itakayoiwezesha nchi kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

WAZIRI JAFO AFANYA ZIARA KATIKA KIWANDA CHA SARUJI TWIGA

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais- Muungano na Mazingira Mhe. Dkt Selemani Jafo amevitaka viwanda vyote Nchini kuiga mfano wa kiwanda cha saruji Twiga kilichopo Manispaa ya Kinondoni Jijini Dar es salaam kwa kutunza na kuhifadhi mazingira.

Aliyasema hayo alipokuwa katika ziara yake ya kikazi ya ukaguzi wa kiwanda hicho cha sementi ambacho kinatumia nishati ya gesi katika uzalishaji wa sementi pamoja na kuanzisha mpango wa kukusanya taka za aina mbalimbali kutoka katika dampo la Pugu Kinyamwezi na maeneo mengine na kuzalisha nishati ya gesi.

Akiwa Kiwandani hapo Mheshimiwa Jafo ametembelea mtambo wa kisasa utakaotumika kuteketeza mifuko ya plastiki iliyokusanywa wakati huu wa kampeni ya kukamata mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku na kupongeza Mkoa wa Dar es salaam kwa kufanikiwa katika suala zima la usimamizi wa katazo la mifuko ya plastiki.

Waziri Jafo akipata maelekezo mafupi kutoka kwa uongozi wa Kiwanda cha Saruji Twiga mara baada ya kutembelea kiwanda hicho katika kukagua uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

> "Twiga sementi ni kiwanda cha mfano wa kuigwa kwani ni kiwanda cha kwanza kuzalisha sementi kwa kutumia nishati ya gesi pamoja na kukusanya taka na kuzichakata kuwa nishati"

"Niwapongeze sana Mkoa wa Dar es Salaam kwa kufanikiwa katika kampeni hii ya kukamata mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku na pia niwashukuru Twiga Cement kwa kukubali kutumia mitambo yao kuteketeza mifuko hiyo"

Katika ziara hiyo Waziri Jafo alipanda mti katika kitalu cha miti cha Kiwanda hiko kama ishara ya kuonesha umuhimu wa upandaji miti na kusisitiza jamii kuhifadhi na kutunza mazingira kwa kupanda miti kila siku.

"Niwapongeze sana kwa juhudi zenu katika utunzaji wa mazingira kwa kuanzisha kitalu hiki cha miti ambapo kwa sasa tuko kwenye kampeni muhimu ya kupanda miti mmeonyesha kitu kikubwa sana".

Naye Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Ufuatiliaji wa Sheria ya Mazingira kutoka NEMC Mhandisi Redempta Samuel amekipongeza kiwanda cha Twiga sementi kwa kukubali kuteketeza mifuko ya plastiki kwa kutumia mitambo yao lakini pia kwa kuchakata taka na kuzalisha nishati ya gesi.

"Nitoe wito kwa Wananchi kutengenisha taka toka zinapozalishwa majumbani ili iwe rahisi zinapokuja kwenye kiwanda hiki ziweze kuchakatwa kwa urahisi na kuzalisha nishati mbadala, tujitahidi tusichanganye takataka kwa sababu kiwanda hiki kina uwezo wa kuzalisha takataka zote ngumu, iwe ni plastiki,mabaki ya mbao, mabaki ya pumba za mpunga na mabaki ya maganda ya korosho."

Katika hatua nyingine Mhe Jafo ameliagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuandaa tuzo maalumu ya Waziri wa Mazingira kwa kiwanda cha Twiga Cement kwa kutunza na kuhifadhi mazingira kutokana na kuendesha shughuli zake kwa kutumia nishati ya gesi lakini pia kwa kuja na mpango wa kukusanya taka, kuzichakata na kuzalisha nishati ya gesi na tuzo nyingine kwa kijana aliyeko Mkoani Mwanza anayetengeneza mabegi ya wanafunzi ya shule kwa tumia mifuko ya sementi iliyotumika.

makala

VIMIMINIKA TAKA KICHOCHEO CHA UCHAFUZI WA MAZINGIRA NA MLIPUKO WA MAGONJWA KWA BINADAMU

Uchafuzi wa mazingira iliyounganishwa na mabomba ya chooni

Maisha yamekuwa na shughuli nyingi sana, hata wanadamu hufika mahali na kusahau kusudi la Mwenyezi Mungu duniani alipokuwa akiumba Ulimwengu na kumkabidhi Mwanadamu mamlaka ya kumiliki na kutawala.

Shughuli hizo nyingi pia zimemfanya mwanadamu kusahau jukumu kubwa alilonalo la kuthamini, kuhifadhi na kutunza Mazingira ambalo kwalo ndio kusudi lake Muumba wetu na ndio msingi mkubwa wa maendeleo.

Ama kwa hakika ukiangalia kwa undani wake shughuli hizo nyingi zifanywazo zikiwemo za migodini, viwandani, hospitalini, mashambani, majumbani na zinginezo ndio chanzo cha taka zinazochafua na kuathiri Mazingira na mwishowe kuzua mlipuko wa magonjwa kama vile kipindupindu, kichocho, 'dengue' na athari kwenye Mazingira kama kuharibika kwa ikolojia za wanyama na mimea pamoja na kuharibu hewa safi kutokana na harufu mbaya.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, taka yenye madhara maana yake ni kitu chochote kigumu, majimaji au cha gesi au taka majimaji ambayo kwa sababu ya athari zake, kiwango chake cha sumu, ulipukaji na kulika/ kubabuka kwake kunadhuru afya, maisha ya binadamu au mazingira.

Katika makala hii leo tutazungumzia taka miminika na jinsi zilivyo kichocheo kikubwa cha uchafuzi wa Mazingira na mlipuko wa magonjwa kwa binadamu.

Unapozungumzia taka miminika kwa tasfiri ya kawaida ni taka zozote zilizo katika hali ya gesi au majimaji zitokanazo na shughuli za viwandani, migodini, biashara, kilimo, majumbani ambazo zinaweza zikawa na madhara kwa mazingira na afya ya binadamu zisipomwagwa au kuhifadhiwa kwa utaratibu maalum ili zisisambae kwa lengo la kuzuia athari zinazoambatana nazo.

Taka miminika zinatokana na shughuli za majumbani na biashara; hizo zinaweza kuwa zilizotokana na majitaka, uoshaji wa vyombo majumbani na kuambatana na mabaki ya vyakula, ufuaji wa nguo kwa sabuni yenye kutengeneza povu, majimaji yenye kemikali yanayotumika kuosha nywele saluni, majimaji ya kuosha matunda au mbogamboga masokoni, maji maji na kuunganishwa kwa mfumo wa majitaka kwenye mfumo wa maji ya mvua kiholela.

Kundi hili la vimiminika taka huweza kupelekea kichocheo kikubwa cha mazalia ya wadudu na bakteria ambao ubeba vimelea vya magonjwa mbalimbali kama vile kipindupindu, dengue, malaria na homa ya tumbo. Wakati mwingine hupelekea mlipuko wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza kutokana na eneo kuathirika na taka vimiminika na kubadilisha hali ya hewa (harufu), joto na mifumo ya ikolojia.

Kama anavyofafanua Ndg. Ramadhan Shausi, Mtaalam wa mazingira kutoka Kanda ya Kusini Mtwara kuhusu Vimiminika taka vitokanavyo na shughuli za viwandani, hospitalini na kilimo;

Bwana Ramadhani anasema shuguli za viwandani huzalisha vimiminika taka vikiwemo, maji taka yatokanayo na mfumo wa utengenezaji bidhaa, mafuta machafu ya kulainishia mitambo, moshi, kemikali zilizochanganyikana na maji n.k. Shughuli za matibabu kutoka Hospitali huzalisha vimiminika taka kama vile majitaka yatokanayo na kusafishia vidonda vya wagonjwa, vifaa tiba, majitaka toka vyooni, mabaki ya madawa ya majimaji na gesi inayozalishwa kutokana na mitambo ya kutibu wagonjwa n.k. Shughuli za kilimo huzalisha vimiminika taka vitokanavyo na matumizi ya viuatilifu, dawa za kupandia, kukuzia na kuuwa magugu hususani madawa hayo yanapochanganyikana na maji au na hewa. Vimiminika taka kutoka katika kundi hili huweza kuleta madhara mbalimbali kwa mazingira na wanyama yakiwemo magojwa ya miwasho, saratani, kuongezeka kwa viumbe vamizi, kubadilika kwa ikolojia ya viumbe, kuharibika kwa tabaka la hewa safi (Ozoni) na kupelekea mabadiliko ya hali ya hewa hususani kuongezeka kwa joto na hata kufa kwa viumbe.

Naye Ndg. Obasanjo Nnwiko ambaye ni Afisa Mazingira Kanda ya Kusini Mtwara amefafanua kuhusu vimiminika taka vitokanavyo na shughuli za migodi. Amesema kundi hili huzalisha vimiminika taka kama vile, tope sumu (tailings), maji asidi (acidic water), mafuta machafu, madini tembo (Heavy metals) gesi sumu (cyanide gas) na majitaka toka vyooni. Madhara ambayo yanaweza kusababishwa na kundi hili la vimiminika taka ni pamoja na miwasho na kubabukwa kwa ngozi, saratani, vifo kwa viumbe hai, mabadiliko ya vinasaba kwa viumbe hai akiwemo binadamu, kuongezeka kwa viumbe vamizi na kubadilika wa ikolojia ya viumbe na mazingira kwa ujumla.

Uchafuzi kwa taka miminika uhalisia wake hautofautiani sana na uchafuzi wa majitaka kwa maana na mtazamo wa uharibifu wa mazingira ambayo kwa hakika yake ni mchanganyiko wa kinyesi, mikojo, uchafu na majitaka yatokanayo na uzalishaji na shughuli za majumbani, shughuli za Asasi au Biashara Mazingira haya huharibiwa sana na matokeo ya shughuli za binadamu zinazozalisha taka vimiminika hizo zinazoambatana wakati mwingine na kemikali isiyo rafiki kwa ardhi na kuharibu ikolojia nzima ya mazingira, hewa safi na afya.

Ni ukweli usiopingika kabisa ya kwamba mazingira safi na salama ni afya, hupendeza machoni, huvutia watalii, huimarisha mimea, hunufaisha viumbe hai na hata ndege wa angani na ndio maana Mungu aliwaumbia binadamu nakuwapa mamlaka ya kuvimiliki na kuvitunza hivyo hatuna budi kufanya hivyo.

Kwa maana hiyo taka vimiminika hizi zinatakiwa kuhifadhiwa kwa utaratibu ulio rafiki utakaowezesha kuhifadhi na kutunza mazingira kwa maslahi mapana ya Nchi na Taifa kwa ujumla.

Tuepuke kumwaga taka vimiminika hovyo ili tuyatunze na kuyahifadhi mazingira yetu.Yatunze mazingira, yakutunze.

makala

FAIDA NA HASARA ZA MAKAA YA MAWE KATIKA MAZINGIRA

Makaa ya mawe ni madini ya nishati ambayo yanapatikana chini ya ardhi kutokana na mkusanyiko wa uchafu wa mimea. Makaa ya mawe ni moja ya aina kongwe ya nishati yenye uwezo mkubwa wa joto inayotumiwa na binadamu. Ingawa ni nishati iliyopo kwa kiwango kikubwa katika uso wa dunia lakini uchimbaji wake ni mgumu sana na wenye gharama kubwa.

Makaa ya mawe ni kati ya nishati zisizoweza kurejeshwa na huharibu mazingira endapo haitatumiwa na kutunzwa kwa usahihi kwani ni moja ya chanzo kikubwa cha ongezeko la joto duniani.

Nishati hii ni muhimu kwani hutoa ajira kwa maelfu ya watu ikiwemo wachimbaji na wamiliki wa migodi, madereva wa malori na vibarua. Vilevile, huingiza na kuongeza kipato kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Pia hutumika katika kuzalisha umeme hasa unaotumika viwandani na kusaidia kupunguza tatizo la uhaba wa umeme.

Licha ya faida zilizoainishwa, bado makaa ya mawe ni nishati inayochafua mazingira kama haitotumika katika uangalizi stahili. Moja ya madhara ya makaa ya mawe ni kusambaa kwa sumu zizalishwazo na makaa ya mawe katika anga na hewa. Sumu hizo ni zebaki, salfadioksidi, kabonimonoksaidi, selenium na arseniki miongoni mwa nyinginezo.

Aidha katika uchangiaji wa uzalishaji wa hewa ukaa na ongezeko la joto duniani,

mkutano wa umoja wa mataifa ulipitisha azimio la kuachana na matumizi ya nishati hii. Hii ni miongoni mwa njia za msingi zaidi za kudhibiti ongezeko la kiwango cha joto duniani ili kisizidi nyuzijoto 1.5 katika kipimo cha Selsiyasi.

Licha ya hayo, uchimbaji wa makaa ya mawe pia unachangia uharibifu wa makazi na mandhari mbalimbali za viumbe, lakini pia hupelekea watu kulazimika kuyahama makazi yao kwa idadi kubwa katika nchi nyingi ambako makaa ya mawe yanachimbwa kwa wingi.

Pia uchimbaji wa makaa ya mawe husababisha vumbi ambalo ni hatari kwa afya ya binadamu kwani husababisha matatizo ya njia ya hewa na hata kupelekea vifo endapo makaa ya mawe yatawekwa sehemu ya wazi bila kufunikwa.

Katika kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi ni muhimu kuzingatia matumizi sahihi ya nishati ya makaa ya mawe. Hii ni pamoja na kutumia njia bora za kuhifadhi nishati hii kwa mfano, kutumia maghala ya kuhifadhia badala ya kuweka mabaki haya katika maeneo ya wazi jambo linalosababisha kusambaa kwa vumbi katika makazi ya watu na kuathiri afya ya binadamu.

Vilevile uchimbaji wa makaa ya mawe uzingatie kiwango kilichoanishwa katika sheria za utunzaji mazingira. Hii ni pamoja na kufanya tathmini na tafiti za athari kwa mazingira kabla na baada ya kubainika kwa madhara yaletwayo na shughuli za uchimbaji wa makaa ya mawe.

Hivyo, ili kukabilina na mabadiliko ya tabianchi na madhara mengine yaletwayo na uchimbaji wa makaa ya mawe, tunahitaji kufanya tathmini na tafiti za athari kwa mazingira na binadamu na kuandaa hatua za usimamizi katika maeneo husika. Aidha, uwekezaji katika nishati mbadala unahitaji kuongezeka ili kuboresha hali ya hewa, kuimarisha afya zetu na kuiokoa sayari. Vilevile, tunatakiwa kuongeza kasi katika hatua za kupambana na mabadiliko ya tabianchi na kuyahusisha malengo ya kuzuia ongezeko la joto duniani kwani tusipoziba ufa tutajenga ukuta.

makala

BANDARI ZISIZOKUWA RASMI NA CHANGAMOTO KWENYE MAZINGIRA

Uhifadhi wa mazingira ni azma ambayo Serikali imeendelea kujiwekea ili kuhakikisha maendeleo ya nchi yetu yanafanyika bila kuathiri mifumo ikolojia na mazingira kwa ujumla. Hii ni katika kuhakikisha maendeo hayo yanafanyika kwa njia ambayo ni endelevu kwa kuzingatia misingi iliyowekwa kupitia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya nchi na ilivyoazimiwa na Tume ya Umoja wa Mataifa ya Brutland (1987) kuwa "maendeleo endelevu ni hali ya kutimiza mahitaji ya vizazi vya sasa bila kuathiri mahitaji ya vizazi vijavyo". Kwa muktadha huo, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), inatekeleza azma hiyo kupitia nyanja mbalimbali za kimaendeleo ikiwemo Sekta ya Uchukuzi kupitia bandari. Bandari ni chachu muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa na nchi jirani.

Pamoja na umuhimu wake kiuchumi, shughuli zinazohusiana na bandari husababisha changamoto mbalimbali za mazingira na kuharibu uhifadhi na hasa bandari zisizo rasmi. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na umwagikaji wa vimiminika hatarishi na taka ngumu kwenda bahari na maeneo ya pwani. Changamoto nyininge ni pamoja na hewa ukaa, moshi na vihatarishi vingine kuchangayika na hewa ambayo ni hitajio la msingi kwa viumbe hai. Pia, bandari zinaweza kuwa vyanzo vya sauti zilizozidi viwango (kelele), hivyo kusababisha madhara kwa viumbe hai na mazingira. Hata hivyo, masuala ya mazingira katika bandari yameendelea kusimamiwa na Baraza ili kuhakikisha mifumo ikolojia iliyopo inalindwa. Hata hivyo, yapo maeneo ambayo hufanya shughuli za kibandari lakini hayapo rasmi.

Hivyo, Baraza limechukua hatua ya kufanya tahtmini ili kubaini changamoto zinazotokana na uwepo wa bandari zisizokuwa rasmi maarufu kama Bandari Bubu. Tathmini hiyo ilikuwa na malengo mahsusi yafuatayo:

- Kubaini maeneo zilipo bandari zisizo rasmi kwa kutumia mifumo ya kijiografia (To map location of the ports through GPS);
- Kufanya tathmini ya mifumo ikolojia inayozizinguka bandari hizo (To assess the ecosystem and associated diversity in areas surrounding informal ports);
- Kubaini shughuli mahsusi zinazofanyika katika kila bandari na kubaini madhara yanayosababishwa na bandari hizo kwenye mazingira (To characterize the activities carried out in the informal ports and assess the resultant environmental impacts);
- Kupendekeza hatua za kuchukuliwa, pamoja na kutoa weledi kwa wadau husika kuhusu uzingatiaji wa matakwa ya Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 (To propose mitigation measures and advise the operators on the legal processes as per EMA of 2004).

Tathmini hii iliyofanywa na Baraza ilibaini kuwepo zaidi ya bandari zisizokuwa rasmi 693 nchi nzima. Kutokana na bandari hizi kutokuwa rasmi, Baraza limekamilisha tathmini kwenye mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam and Mwanza. Kila bandari ilibainika kuwa na changamoto mbalimbali za kimazingira kulingana na eneo bandari ilipo na shughuli zinazoendeshwa katika bandari hiyo. Mfano, baadhi ya bandari zilizofanyiwa tathmini zilibainika kukumbwa na uchafuzi mkubwa unaosababishwa na utupaji taka ngumu kama vile chupa za plastiki, mifuko ya plastiki, masalia ya mbao na misumari ya kutengenezea vyombo vya majini na kinyesi cha binadamu. Taka kama vile taulo za kike (pads) na nepi za watoto (diapers) zilibainika pia kutupwa kwenye fukwe za bandari hizo. Aidha, bandari hizo hazina mifumo na miundombinu ya kutunza mazingira ikiwemo kutokuwepo na vyoo na vifaa vya kuhifadhia taka au vya kutosheleza. Kwa upande mwingine, ilibainika uwepo wa masalia ya vyakula na taka ngumu kutokana na shughuli za kibinadamu zinazofanyika maeneo hayo zikiwemo shughuli za migahawa isiyokuwa rasmi maarufu kama Mama Ntilie. Migahawa hii huchangia kwa kiasi kikubwa uchafuzi wa mazingira maeneo ya bandari. Pia, katika baadhi ya bandari, wadau wengi hutumia fukwe za bahari kwa haja kubwa na ndogo licha ya kuwepo na vyoo vya kulipia vilivyojengwa katika bandari hizo.

Hata hivyo, Bandari nyingine zilizo karibu na mikoko ambapo mikoko hii ni chachu muhimu katika afya na uhai wa viumbe hai kwenye fukwe na bahari, ilibainika kuwa sehemu kubwa ya mikoko hiyo imeshakatwa kupisha miundombinu mbalimbali kama vile ujenzi wa ofisi za muda za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Kwa misingi hiyo, uendelezaji na urasimishaji wa baadhi ya bandari hizi kwa namna nyingine utalazimu ukataji mkubwa wa mikoko.

Vile vile, kutokana na baadhi ya bandari kuwa na kina kifupi, taratibu za kihandisi zitalazimika kufanyika ili kuwezesha vyombo vya majini kutia nanga endapo bandari husika itarasimishwa. Jambo hili huchangangia uharibifu wa mazingira maeneo husika. Katika bandari zenye mazingira ya aina hii, utupwaji wa taka ngumu au umwagaji wa vimiminika usiothibitiwa ulibainika kuwa wa viwango vya chini sana.

Aidha, katika bandari zisizo rasmi mifumo ya maji taka pia sio ya kuridhisha kwani maji machafu kutoka sehemu kama sokoni na maeneo mengineyo hutiririshwa moja kwa moja kuelekea baharini. Vilevile, vyombo vya majini (uvuvi) vinavyohusika kwenye bandari hizi, mfano vya ukanda wa Magharibi wa Bahari ya Hindi, ni vya kawaida na hakuna meli kubwa zinazofikia maeneo haya. Hivyo uchafuzi wa mazingira unaotokana na vyombo vya majini ni wa kiwango cha chini. Hata hivyo, baadhi ya bandari zimeunganishwa kwenye mfumo wa jiji wa maji taka na kuwa na vifaa vya kuhifadhia taka ngumu, lakini taka hatarishi na chuma chakavu bado vinahitaji usimamizi imara zaidi kwani zinatupwa ovyo bila kuzingatia kanuni za mazingira na afya ya binadamu.

Katika tathmini iliyofanyika, Baraza liliiongeza weledi wa waendeshaji wa bandari zote kwa kutoa elimu kuhusu matakwa ya Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 na hatua ambazo zinahitajika kuchukuliwa. Pia, kupitia vikao na mamlaka mbalimbali zinazohusika kama vile Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Baraza lilipendekeza na kuelekeza kuwa endapo bandari husika zitarasimishwa, upembuzi yakinifu (bathymetric study, geotechnical survey, hydrolic – met ocean study) ufanyike ukiambatana na tathmini za athari kwa mazingira. Aidha, mamlaka husika ziweke bayana maeneo mahsusi ya kila bandari kwa kuweka mipaka au alama kwani kwa sasa maeneo hayo hayaoneshi mipaka ya maeneo ya bandari. Hii itasaidia uendeshaji wa bandari husika kutoingiliana na mifumo ikolojia kwenye mazingira.

Maji taka yakiririshwa baharini katika bandari isiyokuwa rasmi ya Kunduchi (Dar es Salaam)

Shughuli za kibinadamu katika bandari isiyokuwa rasmi ya Kipumbwi (Tanga)

makala

VIWANDA ENDELEVU, UCHUMI IMARA KWA MAZINGIRA SAFI NA SALAMA

Viwanda nchini Tanzania ni miongoni mwa sekta kubwa inayoongeza pato la Taifa, sekta hii ni muhimu sana kwani inatoa ajira kwa vijana na kupelekea uchumi wa nchi kukua kwa kasi kubwa. Sekta hii imekuwa kutokana na uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo nchini vya nguo, ngozi, saruji, uchakataji wa chuma na plastiki n.k

Viwanda vinachochea mageuzi ya kimfumo na kijamii katika kilimo na madini. Kuwa na viwanda vingi nchini inachangia uwepo wa bidhaa ndani ya nchi na kupanua wigo wa upatikanaji wa bidhaa na huduma, hii inaongeza uchaguzi katika kukidhi mahitaji kwa watu.

Kilimo ni moja ya sekta inayochangia ukuaji wa viwanda nchini kwani malighafi nyingi zinazotumika katika viwanda vya ndani yanatokana na kilimo, hivyo kilimo ni chachu ya kuwepo kwa viwanda na huchochea wananchi kuhamasika kulima ili kuuza malighafi zao katika viwandani.

Uchumi wa nchi pia hutegemea uwepo wa viwanda kwa kutoa ajira kwa wananchi na ushuru kwa ajili ya maendeleo ya jamii. Kwa mfano kilimo cha pamba kinachochea viwanda kupata malighafi kwa ajili ya kutengeneza nguo hivyo inachangia uwepo wa ajira kwa wananchi wanaojihusisha na kilimo pamoja na uzalishaji viwandani. Hivyo hatuwezi kutenganisha viwanda na kilimo.

Ili kuweza kufikia lengo la uzalishaji ulio thabiti kwa kizazi kilichopo na kijacho ni muhimu kutunza mazingira. Viwanda vinachangia uchumi wa nchi kukua na wananchi kuwa imara kiuchumi na kuweza kukidhi mahitaji yao, lakini kumekuwa na changamoto nyingi kwa wamiliki wa viwanda kutokuzingatia Sheria ya Mazingira.

Utunzaji wa mazingira ni jambo la msingi sana kuzingatiwa kwa ajili kukuza uchumi wa nchi kwani mazingira yakiharibika uchumi endelevu wa Taifa nao utaharibika kwani tutakuwa na Taifa la watu wenye maradhi na ukame.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limekuwa kinara katika kuhakikisha mazingira yanakuwa safi na salama ili kuwezesha wananchi pamoja na wawekezaji kufanya shughuli zao kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni zake. Hii ni kulifanya Taifa kuwa na viwanda endelevu,uchumi imara na mazingira safi na salama kwa maendeleo ya Nchi.

Licha ya kuwepo Sheria ya Mazingira, uharibifu wa mazingira upo wa aina tofauti ukiwamo unaohusisha taka za nyumbani ambazo haziozi kama vile mifuko ya plastiki na mabaki ya vyombo vya plastiki na zile zinazooza kama mabaki ya vyakula na taka hatarishi kama chuma chakavu, taka za hospital n.k.

Taka nyingine ni utiririshaji wa maji machafu yaliyochanganyika na kemikali au vinyesi unaofanywa na baadhi ya viwanda ambalo ni tatizo kwa Serikali licha ya viwanda kutozwa faini kubwa kutokana na tabia hiyo bado changamoto hio imeendelea kuwa mwiba katika jitihada za utunzaji wa mazingira.

Baraza limekuwa likikagua mazingira katika viwanda nchini ili kuhakikisha uzalishaji wa bidhaa katika viwanda hivyo unafanyika bila ya kuathiri mazingira. Changamoto za uchafuzi wa mazingira zipo nyingi kwani malalamiko ni mengi kutoka kwa wananchi juu ya wamiliki wa viwanda kuwa na tabia ya kutiririsha maji machafu yenye kemikali katika mifereji bila ya kuyatibu.

Suala hili limekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wanaoishi maeneo yanayozunguka viwanda kwani wamekua wakipata athari kiafya kutokana na maji hayo kuingia kwenye vyanzo vya maji pamoja na harufu kali ya maji machafu yanayotuama kwenye mifereji hiyo.

Licha ya jitihada nyingi zinazofanywa na serikali kudhibiti uharibifu wa mazingira unaofanywa na viwanda, kwa kutoza faini na kusitisha shughuli zinazofanywa na viwanda ili kupisha ukarabati wa mazingira yanayozunguka viwanda haijasaidia kupunguza tatizo hili.

Hivyo juhudi za kutoa elimu zinapaswa kuongezwa juu ya njia bora za utiririshaji maji taka kutoka kwenye viwanda. Kuna namna mbalimbali za kusimamia maji machafu kwa kuchagua njia ya kutibu maji kwa mfumo unaofaa zaidi nakupunguza athari za uchafuzi wa mazingira na madhara yakiafya kwa wananchi wanozunguka eneo husika. Hivyo mfumo wa kutumia kemikali za kutibu maji, kuweka mitambo maalum ya kukusanya maji taka, ufuatiliaji pamoja na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira kwa mujibu wa sheria.Hii itasaidia kuhifadhi mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na badae kwani Mazingira yetu ni Uhai wetu.

Kauli ya Mazingira Yetu

tu

ALHAMISI 25 AGOSTI,2022

na vifungashio vya viuatilifu ni
nu kuzirudisha chupa hizo katika
elezwa na kuzuia kusambaa kwa

Kauli ya Mazingira Yetu

DUMAA 08 JULAI, 2022

258

Sababu kubwa inayopelekea uharibifu wa hifadhi ya mikoko ni shughuli za kibinadamu zikiwemo kukata miti ya mikoko kwa ajili ya mbao na nguzo, kilimo cha chumvi na uvuvi wa kutumia kemikali. Tuepuke shughuli zinazochangia kuharibu mikoko.

tu

DUMAA 22 JULAI, 2022

nibitiwa hutengeneza makorongo
a ya kilimo na kuyafanya yasiweze
mazingira ili kuepuka uharibifu wa

Kauli ya Mazingira Yetu

JUMANNE 19 JULAI, 2022



13

Mojawapo ya athari za uharibifu wa mazingira ni kupungua kwa uwezo wa ardhi kuzalisha mazao. Hali hii inaweza kusababisha kuwepo kwa janga la njaa.

tu

JUMANNE 09 AGOSTI, 2022

gira ni upotevu wa rasilimali zake
ikolojia zinazotolewa na miti, hivyo
azingira.

Kauli ya Mazingira Yetu

ALHAMISI 14 JULAI ,2022

10

Idadi ya uchafu wa plastiki unaoingia kwenye mifumo ya ikolojia ya majini imeongezeka na inasababisha madhara makubwa kwa afya ya binadamu, uchumi duniani, bayoanuai na kwa hali ya hewa.

Kauli ya Mazingira Yetu

KATUNI



MIKOKO NI MIMEA MUHIMU INAYOSAIDIA KUIMARISHA MIFUMO YA MAZINGIRA YA BAHARI
MIKOKO INA FAIDA NYINGI KATIKA KULINDA MAZINGIRA YETU
TUITUNZE!

KILA MTU ANGETUNZA MAZINGIRA KAMA HIVI INGEPENDEZA SANA
HAKIKA, NA WENGINE WAJIFUNZE, MAANA MAZINGIRA BORA NDIO UHAI WETU
MCHORAJI
Musa Ngarango Jr.
31

JULAI 18, 2022
EID IWE YENYE BARAKA KWETU SOTE HUKU TUKIENDELEA KUTUNZA MAZINGIRA
EID NJEMA, HAKIKA PIA TUSIACHE KUTUNZA MAZINGIRA ILI NAYO YAENDELEE KUTUTUNZA
10
MCHORAJI:
Musa Ngarango Jr.
#MazingiraYetuUhaiWetu

AGOSTI 01, 2022
WATAALAM WANATUSHAURI TULIME KILIMO HIFADHI AMBACHO HUSAIDIA KULINDA MAZINGIRA YETU
NI KWELI, KWANI PIA HUPUNGUZA UPOTEVU WA RASILIMALI UDONGO NA HUONGEZA RUTUBA, TULIME KILIMO HIFADHI ILI KUENDELEA KUTUNZA MAZINGIRA YETU


KUPATA MAJI IMEKUWA TABU, KILA NINAPOCHIMBA NI PAKAVU, HII NI BALAA!
SHIDA YOTE HII IMELETWA NA WAHARIBIFU WA MAZINGIRA, KOSA LETU TULIKAA KIMYA, SASA LAZIMA TUCHUKUE HATUA KULINDA MAZINGIRA YETU

MAJI NI MUHIMU KWA VIUMBE VYOTE DUNIANI IKIWEMO SISI BINADAMU
WANAOHARIBU MAZINGIRA KWA KUKATA MITI HOVYO WANAHATARISHA UWEPO WETU, MAANA BILA MAJI HAKUNA UHAI

HII NI HATARI, TUMEENDA UMBALI MREFU KUTAFUTA MAJI NA BADO TUMEYAKOSA
WANAOHARIBU VYANZO VYA MAJI WANATULEA BALAA
SHIDA HII YA UPATIKANAJI WA MAJI MIJINI NA VIJIJINI INALETWA NA WANAOHARIBU MAZINGIRA, NI LAZIMA JAMII ICHUKUE HATUA


NIMEFURAHI KUONA MRADI TULIOENDA KUOMBA KAZI TAYARI WAMEFANYA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA
UTARATIBU WA KUFANYA TATHMINI KWA ATHARI YA MAZINGIRA NI MZURI, UNASAIDIA SANA KUTUNZA MAZINGIRA YETU
JAMBO HILI LISIPUUZWE, MAANA BILA KUFANYA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA NI HATARI KWA JAMII

Wasiliana nasi;
Mkurugenzi Mkuu,
Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),
Ghorofa ya 6, Jengo la Kambarage, Brabara ya PSPF S.L.P 2724, Dodoma, Tanzania.
Simu: +255 26 296 0098, +255 713 608 930
Barua pepe: dg@nemc.or.tz, Tovuti: www. nemc.or.tz

#MazingiraYetuUhaiWetu

Namba ya Bure: **0800110116**
@nemctanzania
NemcTVTanzania
www.nemc.or.tz